

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

WITO WA KUWASILISHA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni taasisi ya kiserikali inayohusika na usimamizi wa sekta ya mawasiliano ya Kielektroni na Posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT). TCRA inahakikisha kwamba huduma za mawasiliano ambazo ni mawasiliano ya Simu na Intaneti, Utangazaji, huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto zinafuata sheria na kanuni zilizowekwa ili kudumisha usawa, ufanisi na uhakika wa upatikanaji wake kote nchini. TCRA hutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na wadau katika sekta.

Hivyo, TCRA inaalika watafiti wenye ujuzi na uzoefu katika utafiti tumikizi (applied research), kutoka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nje ya nchi, kuwasilisha mapendekezo yao ya kina ya utafiti. Mapendekezo ya utafiti yajikite katika maeneo Matano yakiwamo: mfumo wa kisheria na kanuni unaoongoza sekta ndogo ya mawasiliano ya simu na intaneti, mfumo wa sheria na kanuni za sekta ndogo ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, viwango vya kuridhika kwa walaji, viwango vya kuridhika kwa wateja (watoa huduma za mawasiliano), pamoja na utafiti wa teknolojia chipukizi. Kwa maelezo zaidi kuhusu maeneo ya kuzingatia, mahitaji, vigezo vya tathmini, na njia ya kuwasilisha maombi, tafadhali tembelea tovuti yetu: <https://www.tcra.go.tz>.

Uwasilishaji wa Maombi

Mapendekezo yote na wasifu wa waombaji yawasilishwe kwa Mkurugenzi Mkuu wa TCRA katika nakala laini na ngumu kabla au ifikapo tarehe **30 Aprili 2024 saa 10:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (SAM) kupitia barua pepe: research@tcra.go.tz

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU

Imetolewa tarehe **10 Aprili, 2024**